

## **Maliwazo NDANI YA QURANI TUKUFU**

**Imefasiriwa na**

**Profesa.Ayman Al-asar**

**Hotuba ya Kwanza**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, Msemaji ndani ya Kitabu chake Kitukufu: {**Kwa hakika tunafahamu kuwa moyo wako unaumia kwa yale wanayosema. Basi mtakase sifa njema za Mola wako na kuwa miongoni mwa wanaosujudu. Na muabudu Mola wako mpaka ikufikie yakini**}.

Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba peleka rehema na amani na umbariki Mtume pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na wale wote waliowafuata kwa wema mpaka siku ya kiyama.

**Baada ya utangulizi huo:**

Jambo la kuliwaza ni katika tabia na maadili mema ndani ya Uislamu lakini pia ni tibia ya kiutu na kibinadamu iliyo nzuri ambayo mtu humsaidia mwenzake kushinda huzuni zake na maumivu, mwenye kuzingatia ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuta kuwa uiwazo limepewa nafasi maalum; bali Mwenyezi Mungu Mtukufu amechukuwa jukumu Yeye mwenyewe la kuwaliwaza Mitume yake Mawalii wake na waja wake wema, huyu ndiyo bora wa viumbe *rehema na amani ziwe kwake* pale alipoudhiwa na watu wake na kukuta uzio na dharau kwa watu wake ndipo Mola wake alipomliwaza kwa kauli yake: {**Subiri kwa hukumu ya mola wako kwani wewe upo kwenye uangalizi wetu**} kwa maana subiri kwa hukumu ya Mola wako kwa yale anayokubebesha kutokana na ujumbe wake, na yale balaa iliyopatwa na watu wako, Kwani wewe hakika uko mbele ya macho yetu, tunakuhifadhi, tunakuzunguka na tunakulinda.

wakati moyo wake ulihuzunika kutokana na kuwakataza kuukubali wito wa haki, Mola wetu (AW) alimliwaza kwa kauli yake: { **Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya!** } na kauli yake

**(Huenda labda ukajikera nafsi yako kwa kuwa hawawi Waumini).** kwa maana yeye unaangamia nafsi yako kuhuzunia kwa sababu ya kuwapinga na kuwapuuza haki, basi, Aya hizi na za aya zilizozifanana ziliteremshwa kwa ajili ya kumliwaza na kumfurahi mtume S.A.W

Kama vile, Mola wake Mtukufu alimliwaza akimuelekeza asibebesha nafsi yake kile asichokiweza, Mola Mtukufu akasema: **{Kwa hakika jukumu lako ni kufikisha ujumbe na juu yetu ni hisabu.}** na Mola Mtukufu akasema pia :**{Wewe si mwenye kuwatawalia. }** kwa hiyo usikalifishe nafsi yako jukumu zito sana, kwani kazi yako ni kufikisha na kubainisha, ama kuwaongoza watu ni kazi ya Mwenyezi Mungu peke yake, ambapo Mola Mtukufu anasema: **{Kwa hakika wewe humwongoi umpendaye, lakini Mwenyezi Mungu humwongoa amtakaye. Na Yeye ndiye anawajua zaidi waongokao.}.**

Kama vile, mtazamaji katika Quran Tukufu ataona uliwazaji wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mama wa Nabii Musa A.S, alipoamrishwa kumuweka mtoto wake bahrini, ambapo moyo wake ulijawa na hofu juu ya mwanawe, basi Mwenyezi Mungu akamliwaza na kumtuliza moyo wake, Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: **{ Tulimfunulia mama yake Musa kwa kumwambia: Mnyonyeshe. Na utakapo mkhofia basi mtie mtoni, na usikhofu wala usihuzunike. Hakika Sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya mionganini mwa Mitume}**, kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akamliwaza tena, alipomrudishia mwanawe (AS), Mola Mtukufu anasema: **{Tukamrudisha kwa Mama yake ili mama apate utulivu na wala asihuzunike na apate kufahamu kuwa ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli lakini watu wengi hawafahamu}.**

Kama vile, maliwazo ya Bibi Maryamu (A.S) katika Quran Tukufu, yamekuja **alipokuwa na hali ngumu, na Bibi Maryamu akasema: {Laiti ningekufa kabla ya hali hii na nikawa mwenye kusahaulika}.** Mwenyezi Mungu akamuamrisha mwitaji ili kumtuliza, Akisema: **{Akaitwa kwa sauti iliyotokea chini yake kuwa usihuzunike kwani Mola wako amefanya chini yako mto mdogo wa maji \* Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu \* hivyo kula na kunywa nafsi yako itulie}.**

## **Hotuba ya Pili.**

Shukrani zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe vyote, sala na salamu zimwendee Mtume wetu wa mwisho, Muhammad (SAW) na familia yake na Maswahaba yake wote.

Kwa hakika aina za maliwazo ni nyingi sana, mionganini mwazo ni: Kuliwaza kwa mali, kuliwaza kwa kutoa nasaha, kuliwaza kwa hisia, kuliwaza kwa maombi, na Quran Tukufu imetubainisha maliwazo ya mtu mwema kwa Nabii Musa (A.S) wakati Nabii Musa alitoka akiwa anaogopa watu wake, na ikatusimulia kisa chake na Firauni, na Mwenyezi Mungu akamliwaza kwa kusema: **{Wala usiogope umenusurika kwa watu madhalimu}**, kama vile Quran imetubainisha kuliwaza kwa Malaika A.S kwa Mtume Luut (A.S) alipoogopa watu wake, Malaika wakamwambia: **{Usiogope wala usihuzunike kwani sisi ni wenyewe kukunusuru wewe na watu wako}**.

Na Mtume wetu Muhammad (SAW) ametuhimiza kushikilia maadili haya bora, pale aliposema: “*Mtu ye yeyote mwenye ziada ya mnyama basi ambebee yule asiye na mnyama, na mwenye ziada ya maandalizi basi na ampe asiye na maandalizi*”.

Na anasema pia S.A.W: “*Yeyote mwenye kutaka Mwenyezi Mungu amuokoe na shida za siku ya Kiyama basi amsaidie mwenye matatizo au kumuondolea matatizo yake*”.

Pia Mtume S.A.W amesema: “*Mwenyezi Mungu bado yupo kwenye mahitaji ya mja madamu mja naye yupo kwenye mahitaji ya ndugu yake*”.

Mtume wetu Muhammad S.A.W alipotulia katika mji wa Madina, Maswahaba walimwuliza: “*Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hatujaona watu wanaotoa kwa wingi, wala kuliwaza sana zaidi ya wenyehi tuliofikiwa kwao – wakimaanisha watu wa Madina*”.

Kama vile Mtume S.A.W alivyowasifu watu wa Ash-Ary kwa kujipamba kwao na tabia hii bora, pale Mtume aliposema: “*Hakika watu wa Ash-Ary wanapomaliza chakula chao katika vita au kupungua chakula cha watoto wao huko Madina, basi*

*hukusanya walivyo navyo kwenye nguo moja, kisha wanagawana kati yao ndani ya chombo kimoja kwa usawa, basi wao ni katika mimi na mimi ni katika wao”.*

Hivyo, sisi ni wenyewe kuhitajika sana kujipamba na tabia ya kuliwazana kati yetu mpaka ienea roho ya undugu na kuimarika kwa mahusiano mema kwenye jamii na kufunikwa na umoja pamoja na kupendo kati yetu.

**Ewe Mwenyezi Mungu ziunganishe nyoyo zetu na utufanyie mazuri yaliyopo  
kati yetu.**